# DONDOO ZA MHE. SAMIA SULUHU HASSAN, RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA BAADA YA KUFANYA MAZUNGUMZO RASMI NA MHE. EVARISTE NDAYISHIMIYE, RAIS WA JAMHURI YA BURUNDI BUJUMBURA, TAREHE 16 JULAI, 2021

*Mheshimiwa Evariste Ndayishimiye,*
*Rais wa Jamhuri ya Burundi;*

*Waheshimiwa Mawaziri wa Burundi na Tanzania mliopo;*

*Waheshimiwa Viongozi wengine wa Serikali zetu mbili mliopo;*

*Ndugu Wana-Habari;*

## UTANGULIZI

- Kwa mara nyingine, napenda nikushukuru sana, kaka yangu, Mheshimiwa Rais Evariste Ndayishimiye, kwa kunialika kufanya Ziara hii ya Kiserikali nchini Burundi.

Nikushukuru pia kwa makaribisho mazuri mliyonipatia mimi pamoja na ujumbe wangu. Ahsanteni sana.

***Ndugu Wana-Habari;***

- Nimekuja Burundi kwa sababu kubwa nne. *Kwanza,* kujitambulisha kufuatia Kifo cha aliyekuwa Rais wetu, Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Kama unavyofahamu, ukiwa mgeni kwenye Mtaa ama Mpangaji mpya kwenye nyumba, ni lazima kujitambulisha.

- *Pili,* nimekuja Burundi kutoa shukran kwa kushiriki nasi kwenye kipindi cha msiba mkubwa uliotupata Watanzania wa kuondokewa na Rais wetu. Kwenye Mazishi ya Kitaifa, Burundi iliwakilishwa na Makamu wa Rais, Mheshimiwa Prosper Bazombanza. Mlitufariji sana. Tunawashukuru sana. Kama msemo wa Kiswahili usemavyo, *"Akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki wa kweli".*

- *Tatu,* nimekuja Burundi kuwapongeza. Tarehe 1 Julai, mwaka huu, mlisheherekea miaka 59 ya Uhuru. Kaka yangu Rais Ndayishimiye alinialika kuhudhuria Sherehe hizo. Hata hivyo, kwa sababu ya majukumu niliyokuwa nao wakati huo, sikuweza; badala yake nilimtuma Waziri Mkuu aniwakilishe. Najua aliniwakilisha vyema; lakini nilipopata mwaliko tena, nikaona ni fursa nzuri ya mimi pia kuja kuwapongeza. Hongereni sana ndugu na rafiki zetu. Burundi ya mwaka 1962 sio sawa na Burundi ya leo.

- Sababu ya nne, ambayo pengine ni muhimu zaidi, ni kwamba, nimekuja Burundi kwa lengo la kukuza na kuendeleza uhusiano mzuri wa kidugu, kirafiki na ujirani mwema uliopo kati ya mataifa yetu mawili. Kama mnavyofahamu, nchi zetu mbili zina uhusiano mzuri wa enzi na enzi. Hivyo basi, kwa kuwa mimi ni Rais mpya wa Tanzania, nimeona kuna umuhimu wa kuja Burundi

kukutana na kaka yangu, Mheshimiwa Evariste Ndayishimiye, ili tubadilishane mawazo ya namna ya kukuza zaidi uhusiano kati ya mataifa yetu mawili.

- Mtakavyokumbuka pia, baada ya kaka yangu, Rais Ndayishimiye kuwa Rais, ziara yake ya kwanza nje ya nchi aliifanya Tanzania mwezi Septemba, 2020, ambapo alikutana na Mtangulizi wangu Hayati Rais Dkt. Magufuli. Na hii ni ishara kwamba nchi zetu ni marafiki na zina uhusiano mzuri.

## MUHTASARI WA MAZUNGUMZO

*Ndugu wana-Habari;*

- Kama alivyosema kaka yangu Rais Ndayishimiye, muda mfupi uliopita, tumefanya naye mazungumzo.

ameyaeleza. Kwa hiyo, mimi nitaongeza maneno machache kukazia kile ambacho tayari amekieleza.

- Kwa ujumla, mazungumzo yetu yalijikita katika kukuza ushirikiano wa kiuchumi kati yetu. Kama mjuavyo, katika dunia ya sasa, uhusiano na ushirikiano baina ya mataifa umejikita zaidi kwenye masuala hayo. Hivyo, nasi tumejadili kwa kirefu suala hilo, hususan namna ya kukuza zaidi biashara na uwekezaji.

- Takwimu zetu za sasa zinaonesha kuwa biashara kati yetu imeongezeka kutoka **shilingi bilioni 83.9** mwaka 2015 hadi kufikia **shilingi bilioni 200.1** mwaka 2019. Kuhusu uwekezaji, Kituo cha Uwekezaji Tanzania kimesajili miradi **18** kutoka Burundi yenye thamani ya **Dola za Marekani milioni 209.42** ambayo imetoa ajira zipatazo **3,544**, ukiwemo mradi mkubwa wa kiwanda cha mbolea

unaojengwa na Kampuni ya ITRACOM wenye thamani ya **Dola za Marekani milioni 180.**

- Kwa upande wa Tanzania, kama mnavyofahamu, hapa Burundi zipo kampuni nyingi za Tanzania ambazo zimewekeza. Baadhi ya Kampuni hizo ni Azam Ltd; Azania Group, Interpetrol, Ndaki Contractors Co. Ltd; Tanzania Bile Acids Ltd na Benki ya CRDB. Hata hivyo, tumesema kwamba, kiwango cha biashara na uwekezaji kati yetu bado ni kidogo sana ukilinganisha na fursa zilizopo, ukaribu na uhusiano mzuri tulionao.

- *Hivyo basi, tumekubaliana kuendelea kushirikiana kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji kwenye nchi zetu kwa kuondoa vikwazo vya kodi na visivyo vya kodi, ikiwemo kuharakisha ujenzi wa Kituo cha Pamoja cha Huduma za Mpakani kwenye Mpaka wetu wa Manyovu/Mugina. Tumekubaliana pia kuendelea*

*kuwahamasisha wafanyabiashara wetu kuchangamkia fursa zilizopo kwenye nchi yetu. Na katika hilo, napenda kutumia fursa hii kuwakaribisha wafanyabiashara wa Burundi kuwekeza Tanzania kwenye sekta mbalimbali, ikiwemo viwanda, kilimo, madini, utalii, n.k.*

## MIUNDOMBINU YA USAFIRI NA UCHUKUZI

*Ndugu wana-Habari;*

- Kama mnavyofahamu, ni vigumu kukuza biashara na uwekezaji bila kuimarisha miundombinu ya usafiri na uchukuzi. Kwa kuzingatia hilo, mazungumzo yetu yalijikita pia katika kutafuta mbinu za kuimarisha miundombinu ya usafiri na kuboresha huduma za uchukuzi. Hivyo basi, tumekubaliana kuendelea kushirikiana kujenga Barabara zinazounganisha nchi zetu, ikiwemo ile ya Nyakanazi – Kasulu – Manyovu/Rumonge – Gitaza.

Aidha, kama mnavyofahamu, nchi zetu zimesaini makubaliano ya kujenga Reli ya Uvinza – Msongati – Gitega. Hivyo, tumewaelekeza Mawaziri wetu wa Fedha na Uchukuzi, kushirikiana kutafuta fedha ili kuharakisha ujenzi wa reli hiyo.

- Sambamba na hilo, nimemweleza Mheshimiwa Rais Ndayishimiye kuwa kwa upande wetu Tanzania tunaendelea na ujenzi wa reli kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma ambayo itakwenda hadi Tabora; na kisha Kigoma, ambako itaunganika na reli ya Uvinza – Msongati – Gitega. Aidha, tunafanya upanuzi wa Bandari yetu ya Dar es Salaam pamoja za Kigoma, Kalema, Kasanga na Kabwe kwenye Ziwa Tanganyika; ambazo ni kiungo muhimu cha usafiri kati ya Tanzania na Burundi. Vilevile, tumeanza ukarabati wa meli ya kubeba mafuta **tani 350** ya MT. Sangara, pamoja na ujenzi wa meli mpya

mbili; moja ya kubeba abiria **400** na mizigo **tani 600,** na nyingine itakuwa ya kubeba mizigo peke yake **tani 2800.** Nimeipongeza pia Burundi kwa kupata mkopo kutoka AfDB kwa ajili ya upanuzi wa Bandari ya Bujumbura.

- Vilevile, tumezungumzia ombi la Burundi kutaka eneo la kuhifadhi mizigo katika Bandari Kavu ya Kwala. Nimemwarifu Mheshimiwa Rais Ndayishimiye kuwa tumetenga hekta 10, takriban **mita za mraba 10,000,** kwa ajili ya Burundi. Kilichobaki ni kwa wataalam wa pande zetu mbili kukutana na kukamilisha taratibu zilizobaki.

- Hivyo basi, nawakaribisha wafanyabiashara wa Burundi kuendelea kutumia Bandari ya Dar es Salaam kupitisha mizigo yenu. Nafahamu, kwa sasa, takriban asilimia 95 ya mizigo ya Burundi inapitia Tanzania, ambapo mwaka

jana mlipitisha tani **476,809.** Tunatamani kuona mizigo yote ya Burundi ikipita Tanzania.

- Kuhusu usafiri wa anga, kama mnavyofahamu, kutokana na mlipuko wa CORONA, mwezi Machi 2021, Shirika la Ndege la Tanzania lilisitisha safari kati ya Tanzania na Burundi. Hata hivyo, maandalizi ya kurejesha safari yanaendelea. Hivyo basi, nawaomba wananchi wa Burundi kuendelea kutumia ndege za shirika hilo, ambalo limeanza pia kufanya safari za kwenda China.

**SEKTA YA NISHATI**

- Tumejadiliana pia kuhusu umuhimu wa kuharakisha utekelezaji wa mradi wa kuzalisha umeme **Megawati 80** pale Rusumo pamoja na marafiki zetu wa Rwanda. Kama mnavyofahamu, nishati ya umeme ni kichocheo muhimu cha kukuza uchumi, ikiwemo kuvutia wawekezaji.

- Hivyo, nimeipongeza Burundi kwa kutekeleza Mradi wa Umeme wa Mulembwe utakaozalisha **Megawati 48.** Aidha, nimemweleza Kaka yangu Rais Ndayishimiye kuwa na sisi Tanzania tunatekeleza Mradi mkubwa wa umeme wa Bwawa la Nyerere utakaozalisha **Megawati 2115**. Mradi huu utakapokamilika, mwaka 2022, utaifanya nchi yetu iwe na umeme mwigi wa ziada, ambao tutakuwa tayari kuwauzia ninyi ndugu zetu wa Burundi, endapo mtahitaji.

## SEKTA YA MAWASILIANO

*Ndugu wana-Habari;*

- Kama mnavyofahamu, dunia hivi sasa ipo kwenye mapinduzi ya nne ya viwanda ambayo yanaongozwa na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano. Shughuli nyingi duniani zinafanyika kwa njia ya mtandao. Nchi za Afrika

hazipaswi kuwa nyuma. Ni lazima ziende sambamba na maendeleo hayo.

- Kwa kuzingatia hilo, kwenye mazungumzo yetu ya leo na kaka yangu Rais Ndayishimiye, tumejadiliana kuhusu namna ya kukuza ushirikiano kwenye eneo hilo. Kama mnavyofahamu, Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano (*Tanzania National Fibre Broadband Backborne*) umefika hadi Burundi, ambapo uwezo wake ni **Gigabaiti 100**. Mwaka 2019, Tanzania na Burundi, kupitia *Burundi Backborne System,* tulisaini ya Makubaliano ya kuruhusu Burundi kutumia Mkongo huo. Hata hivyo, kwa sasa Burundi inatumia **Gigabaiti 2.6** tu.

- Hivyo basi, tumekubaliana kuihimiza taasisi husika za pande zetu mbili kushirikiana ili kuongeza matumizi ya huduma hiyo ya mawasiliano. Endapo kuna changamoto

yoyote, tumewataka wataalam wetu wa pande zote mbili wakutane, ili kuondoa vikwazo hivyo.

**SEKTA YA MADINI**

- Sekta ya madini ni eneo jingine ambalo tumekubaliana kukuza ushirikiano. Kama mnavyofahamu, mataifa yetu yamebarikiwa kuwa na utajiri mkubwa wa rasilimali hiyo. Mathalan, Burundi ina hazina kubwa ya madini ya *nickel* pale Msongati; na sisi tunayo madini hayo pale Kabanga. Maeneo hayo yapo karibu.

- Hivyo basi, tumekubaliana kushirikiana. Na katika hilo, nimemwarifu Mheshimiwa Rais Ndayishimiye kuwa mwezi Januari, 2021, Tanzania ilisaini makubaliano na Kampuni *LZ Nickel Ltd* kuchimba madini na kujenga Kiwanda cha Kusafisha na Kuchenjua madini hayo ya Nickel. Hivyo, nimeshauri kuwa, badala ya Burundi

kusafirisha madini hayo yakiwa ghafi wayalete kwenye Kiwanda chetu kitakachojengwa Kahama ili kuyaongeza thamani. Lakini zaidi ya hapo, narudia kuwakaribisha wafanyabiashara wa Burundi kuuza madini kwenye Masoko ya Tanzania na halikadhalika kuja kuwekeza kwenye sekta ya madini (kwenye uchimbaji pamoja na kujenga mitambo ya kusafisha na uchenjuaji).

## MAENEO MENGINE YA USHIRIKIANO

*Ndugu wana-Habari;*

- Maeneo mengine tuliyoyajadili ni pamoja na kuongeza ushirikiano kwenye masuala ya ulinzi na usalama, hususana kwenye maeneo ya mipaka yetu pamoja na kushughulikia masuala ya Wakimbizi, ambapo kwa sasa idadi ya wakimbizi wa Burundi waliopo Tanzania ni **140,706.** Tumekubaliana pia kuimarisha ushirikiano

kwenye sekta za kilimo; uvuvi; ufugaji; utalii; utunzaji maji na mazingira; sanaa michezo na utamaduni.

- Na kama mlivyoshuhudia, baadhi ya maeneo hayo Mikataba yake ya ushirikiano tumeisaini hivi punde. Lakini, nikiri kuwa nimefurahishwa sana na kusainiwa kwa Mikataba ya Ushirikiano ya ufundishaji wa lugha za Kiswahili na Kifaransa kwenye nchi zetu pamoja na masuala ya afya. Kama mnavyofahamu, lugha ni nyenzo muhimu ya kukuza ushirikiano; na kwa bahati nzuri Kiswahili na Kiingereza zote ni lugha za kimataifa.

- Kwa upande wa afya, Mkataba wa Ushirikiano uliosainiwa ni muhimu sana. Kama mavyofahamu, masuala ya afya au magonjwa hayajui mipaka. Mathalan, hivi sasa nchi zetu na dunia kwa ujumla inakabiliwa na ugonjwa wa CORONA. Ili kuukabili ugonjwa huo ni

lazima tushirikiane. Lakini kuhusu afya pia, napenda kutumia fursa hii kuwaarifu ndugu na marafiki zetu wa Burundi kuwa, kwenye miaka ya hivi karibuni, sisi Tanzania tumewekeza sana kwenye masuala ya tiba za kibingwa na bobezi, hususan kwa magonjwa ya moyo. Taasisi yetu ya Moyo ya Benjamin Mkapa ina vifaa vya kisasa na wataalam wabobezi; na ninafahamu baadhi ya raia wa Burundi wametibiwa kwenye taasisi hiyo. Hivyo basi, tunawaomba ndugu zetu wa Burundi mwendelee kuja kutibiwa kwenye Taasisi hiyo, ambayo kwa sasa inasifika kuwa miongoni mwa Taasisi zinazotoa huduma bora za matibabu ya moyo Barani Afrika.

## UHUSIANO WA KIMATAIFA

- Wakati wa mazungumzo yetu, tumepata pia fursa ya kubadilishana mawazo kuhusu masuala ya kimataifa. Kama mnavyofahamu, mbali na ushirikiano wetu katika

nyanja za kitaifa, Tanzania na Burundi tunashirikiana vizuri kimataifa, hususan kupitia Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Nchi za Maziwa Makuu, Umoja wa Afrika na Umoja wa Mataifa; ambako mara nyingi tumekuwa na misimamo inayofanana.

- Hivyo basi, tumekubaliana kuendeleza ushirikiano wetu kimataifa. Na katika hilo, nimemwakikishia Mheshimiwa Rais Ndayishimiye kuwa Tanzania itaendelea kupaza sauti ya kutaka Burundi iondolewe vikwazo. Aidha, tutaendelea kuzishawishi nchi nyingine Wanachama wa SADC kukubali ombi la Burundi la kujiunga na Jumuiya hiyo.

## HITIMISHO

- Kwa kifupi sana, hayo ndiyo tuliyoyajadili mimi na Kaka yangu, Mheshimiwa Rais Ndayishimiye. Narudia kumshukuru kwa kunialika kutembelea nchi yake. Namwahidi, Tanzania chini ya uongozi wangu, itaenzi, kudumisha na kuendeleza uhusiano wa kidugu, kirafiki na ujirani mwema kati ya mataifa yetu mawili. Mwisho lakini sio umuhimu, napenda kumwalika kaka yangu naye, muda utakaporuhusu afanye Ziara rasmi ya Kiserikali nchini Tanzania.

**"Ahsanteni sana kwa Kunisikiliza"**